HALMASHAURI YA MJI KONDOA

MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 09/02/2023 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA.

**Waliohudhuria**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed A.Kiberenge | -D/K/Mjini | - M/kiti |
| 2. | Mhe. Besela I. Maunga | -D/V/Maalum | - M/M/kiti |
| 3. | Mhe. Juma I. Ng'ungu | -D/Kolo | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zainabu H. Hemed | -D/Chemchem | - " |
| 5. | Mhe. Abushehe I. Mbuva | -D/Kingale | - " |
| 6. | Mhe. Issa I. Kambi | -D/Kilimani | - " |
| 7. | Mhe. Jafari M. Ganga | -D/Suruke | - " |
| 8. | Mhe. Rachel M. Sombida | -D/V/Maalum | - " |
| 9. | Mhe. Kulwa S. Pazi | -D/Serya | - " |
| 10. | Mhe. Fatuma I. Issa | -D/V/Maalum | - " |
| 11. | Mhe. Hajat Ramla H. Abedi | -D/Bolisa | - " |
| 12. | Ndg. Annette T. Nara | -Kny.Mkurugenzi | - Katibu |

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Rahab Sanga | -Kaimu Mkuu Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 2. | Ndg. Shabani N. Sued | -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria |
| 3. | Ndg. Esther Komba | -Kny. Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu |
| 4. | Ndg. Hassan Kiseto | -Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 5. | Eng. Jeremia Longido | -Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini. |
| 6. | Ndg. Irene Mosha | -Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii |
| 7. | Ndg. Hassan Mtamba | -Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 8. | Ndg Lucy J. Timba | -Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu |
| 9. | Ndg.Sekela Mwasubila | -Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Ndg. Alfred Chakalike | -Kny.Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira. |
| 11. | Ndg. Ramadhan J. Hamis | -Kny.Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira |
| 12. | Dkt. Sisti A. Mosha | -Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe |

**KAMATI YA ULINZI NA USALAMA**

1. Ndg. Ezra Ndalima - DSO
2. SSP. Zephania Neligwa - DPO
3. SP. Fadhiri Ngongite - O/C King'ang'a
4. ASI.Mustafa Kapingu - DIO
5. Inspector I.B. Chanyika - DFO
6. SSGT. Andrew S. Katama - M/JA(W)
7. SSP. Yowabu Lusatila - OCD
8. Ndg. Michael Sanga - DBC

**MAAFISA TARAFA**

1. Ndg. Ally R. Mbena - Afisa Tarafa ya Kondoa Mjini
2. Ndg. Fred J. Bangule - Afisa Tarafa ya Kolo

**VYAMA VYA SIASA**

1. Ndg. Hija Bakari Suru - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi
2. Ndg. Ibrahimu S. Mpwapwa - Katibu wa Chama Cha Mapinduzi
3. Ndg. Adam. H. Mtopa - Katibu wa Mbunge

**WAANDISHI WA HABARI**

1. Ndg. Jafari Mohamed
2. Ndg. Brighton Kimaro
3. Ndg. Nizari Mafita
4. Ndg. Michael Samwel

**Sekretarieti**

1. Ndg. Rosemary M. Mnguli
2. Ndg. Tatu N. Jabily

**MUHTA NA 15/2022/2023 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote kwenye kikao aliwashukuru kwa mahudhurio yao mazuri. Alifungua kikao saa 5:16 asubuhi baada ya kujiridhisha kutimia kwa akidi ya wajumbe.

**MUHTA NA 16/2022/2023 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa na kuridhiwa na wajumbe:

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 02/11/2022.
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Mji
5. Kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara kutoka Kamati za kudumu za Halmashauri na Kamati zisizo za kudumu.
   i. Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
   ii. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira
   iii. Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI.
   iv. Kamati ya Fedha na Utawala.
6. Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi
7. Masuala ya kiutumishi
8. Kufunga kikao.

**MUHT. NA 17/2022/2023 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 02/11/2022**

Baada ya kusomwa na kutokuwa na masahihisho yoyote muhtasari wa kikao cha tarehe 02/11/2022 ulithibitishwa na kusainiwa na kuwa nyaraka halali ya Halmashauri ya Mji Kondoa.



CamScanner

**MUHTA NA 18/2022/2023 MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MWENYEKITI NA MKURUGENZI**

**Swali kutoka kwa Mhe. Jafari Ganga wa Kata ya Suruke.**

Alihoji kuhusu mipaka (GN) ya maeneo ya Mitaa ya Ausia na Mulua katika Halmashauri ya Mji Kondoa.

Menejimenti ilipokea suala hilo kwa ajili ya ufuatiliaji wa GN inayotambua mipaka halisi ya mitaa yote ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

Pia mjumbe alipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza ambapo aliuliza kuhusu Halmashauri ya Mji Kondoa kutambua GN namba mbili inayotambua makorido na mpaka halisi kati ya mitaa na pori tengefu. Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri inafahamu GN namba mbili iliyokuwa ikitumika kabla ya mgawanyo wa Halmashauri kufanyika na iliyotumika katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uchaguzi Mkuu. Hata hivyo, Menejimenti ilipokea suala hilo kwa ajili ya kulifanyia kazi kwa kujiridhisha na mipaka halisi ya maeneo hayo.

**Swali kutoka kwa Mhe, Ramla Abedi wa Kata ya Bolisa.**

Alihoji kuhusu uendelezaji wa kisima cha maji kilichochimbwa katika Kata ya Bolisa na kuachwa bila ya uendelezo wowote wa usambazaji wa maji kwa wananchi wa Kata hiyo ambapo wananchi wake wana uhitaji mkubwa wa maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. Menejimenti imepokea suala hilo kwa ajili ya kufanya mawasiliano na Meneja wa Mamlaka ya Maji (RUWASA) ili kutoa ufafanuzi juu ya suala hilo na pia wataalikwa kwenye vikao vya baraza ili kuja kutoa ufafanuzi wa masuala yanayohusu miradi ya maji.

**MUHT NA 19/2022/2023 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA KUTOKA KAMATI ZA KUDUMU NA ZISIZO ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA – DISEMBA, 2022/2023.**

Wenyeviti wa Kamati za kudumu na zisizo za kudumu waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na Divisheni na Vitengo zilizo chini ya Kamati zao kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2022 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika kikao cha Baraza la Waheshiwa Madiwani. Kamati zilizowasilisha taarifa ni kama zifuatavyo:-



CamScanner

## I. Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya aliwasilisha taarifa ya Kamati yake mbele ya wajumbe wa kikao ambapo ilielezwa kuwa Kamati ina jumla ya Divisheni na Vitengo nane ambazo ni Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Divisheni Elimu ya Awali na Msingi, Divisheni ya Elimu Sekondari, Divisheni ya viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taarifa ya iCHF na Taarifa ya TASAF. Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 17/01/2023 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili na kisha ilihojiwa kuhusu vyama vya ushirika kutokuhusishwa katika ugawaji wa mbolea kwa wananchi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa vyama vilivyopo katika Halmashauri ya Mji Kondoa ni Mkombozi Soko Kuu SACCOS, Kondoa Teachers Saccos na Kicheta SACCOS ilielezwa kuwa mazungumzo yalifanyika na ilionekana SACCOS kutokuwa na uwezo wa kusambaza mbolea hiyo kwa kuwa SACCOS hizi zinahusika na masuala ya kifedha ya kuweka na kukopa hivyo jukumu hilo lilitakiwa kufanywa na vyama vya Ushirika vya wakulima. Hata hivyo, jukumu hilo lilikwama kutokana na kuchelewa kupatiwa taarifa kwa wakati za usimamizi wa ugawaji wa mbolea pamoja na mawakala.

Pia wajumbe walihoji kuhusu sababu inayopelekea wananchi wengi kutojiunga na Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHF). Ilifafanuliwa kuwa hii imetokana na ucheleweshaji wa kadi za wananchama pamoja na kutokuwasilishwa kwa wakati kwa fedha za iCHF kutoka ngazi ya Mkoa sababu inayopelekea wananchi kukosa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha, Menejimenti ilihojiwa kuhusu mikakati iliyowekwa ya kuhakikisha kuwa wananchi wanajiunga na Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHF). Ufafanuzi ulitolewa kuwa uhamasishaji wa wananchi unaendelea kufanyika kupitia Mratibu wa iCHF ngazi ya Halmashauri. Pia ilishauriwa Waheshimiwa Madiwani kusaidia kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHF) katika maeneo yao.

Pia ilihojiwa kuhusu sababu zinazopelekea wagonjwa wanaopatiwa matibabu ya upasuaji katika hospitali ya Mji Kondoa wenye ugonjwa wa henia kwa wanaume vidonda hivyo kuachia (kufumuka). Ufafanuzi ulitolewa kuwa sababu kubwa inayopelekea kuachia (kufumuka) kwa



CamScanner

vidonda hivyo ni wagonjwa wenyewe kutokuzingatia masharti wanayopewa na Daktari baada ya kufanyiwa upasuaji. Aidha, ilielezwa kuwa Halmashauri ya Mji Kondoa haijapokea taarifa rasmi kuhusu tatizo hilo.

Wajumbe walihoji kuhusu namna Maafisa Elimu Kata wanavyohusika katika kusaidia kuwarejesha wanafunzi watoro shuleni. Ufafanuzi ulitolewa kuwa Maafisa Elimu Kata ni wajibu wao kuhakikisha kuwa wanafunzi watoro wote wanarejea shuleni kwa kushirikiana na Watendaji wa Kata na Mitaa na taarifa kuwasilishwa kwa Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari. Pia ilishauriwa watendaji kupatiwa motisha kwa ajili ya kuwafuatilia wanafunzi hao ili kuwarejesha shuleni. Ufafanuzi ulitolewa kuwa ofisi ya Mkurugenzi imekuwa ikisaidiana na watendaji hao na kuwawezesha katika zoezi la ufuatiliaji wa wanafunzi watoro.

Vilevile, wajumbe walishauri kuwa Halmashauri ya Mji kutunga Sheria ndogo ambazo zitatumika kuwabana wazazi ili kuhakikisha wanawafuatilia watoto wao kwenda Shuleni, pamoja na Menejimenti kutoa maelekezo kwa Maafisa Elimu Kata kushiriki kwa ukaribu katika kuhakikisha utoro unapungua shuleni. Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**II. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira**

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya Kamati yake mbele ya wajumbe wa kikao ambapo alieleza kuwa Kamati hii inajumuisha Divisheni moja na Vitengo viwili ambazo ni Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini, Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira na Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira. Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 18/01/2023 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kisha walihoji kuhusu sababu iliyopelekea kusimama kwa ujenzi wa mradi wa Zahanati ya Ausia na Mulua. Ufafanuzi ulitolewa kuwa miradi hiyo imesimama kutokana na ufinyu wa bajeti kwa fedha za mapato ya ndani ambapo kwa sasa Halmashauri imepanga kupeleka fedha katika zahanati ya Choka na Hachwi pamoja na kukamilisha ujenzi wa Stendi ya Bicha na baada ya kukamilika kwa miradi hiyo ndipo miradi ya ujenzi ya Ausia na Mulua itapelekewa fedha za kukamilisha ujenzi.



CamScanner

Aidha, wajumbe walihoji kuhusu taratibu zitakazotumika za kuvunjwa kwa vibanda vitavyojengwa katika stendi mpya ya Bicha baada ya mkataba wa vibanda hivyo kuisha. Ufafanuzi ulitolewa kuwa mkataba wa ujenzi wa vibanda hivyo unaeleza wazi kwamba vibanda vitakavyojengwa ni vya muda mfupi. Hivyo, mradi wa TACTIC utakapoanza kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kudumu vibanda hivyo vitaondolewa.

Pia wajumbe walihoji kuhusu kutokulipwa kwa kifuta jasho kwa wananchi ambao mazao yao yaliliwa na wanyama. Ufafanuzi ulitolewa kuwa utaratibu wa kulipa kifuta jasho unazingatia ukubwa wa eneo na umbali wa shamba kutoka kwenye mpaka wa hifadhi ambapo ilielezwa kuwa umbali huo usipungue nusu kilomita hadi kwenye shamba. Hivyo wananchi waliolipwa ni ambao mashamba yao yanazidi ukubwa wa nusu ekari na yamezingatia vigezo vya umbali kutoka kwenye hifadhi.

Aidha, wajumbe walihoji kuhusu ucheleweshaji wa urejeshaji wa fedha za uzoaji wa taka zinazorejeshwa katika mitaa pia asilimia sitini ya fedha zinazorejeshwa ni kidogo na hazitoshi katika kusimamia suala la usafi wa mazingira kwenye Mitaa. Ufafanuzi ulitolewa kuwa Menejimenti haijapokea taarifa ya mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo zinazorejeshwa kwenye mitaa hiyo. Hivyo, kiasi hicho cha fedha kinachopelekwa kinatosha kutekeleza shughuli zilizopangwa. Pia ilielezwa kuwa fedha hizo zinazopelekwa katika mitaa hiyo kama hazitoshi katika shughuli zilizopangwa basi Mtaa husika uandike barua kwenda kwa Mkurugenzi kuomba kuongezewa fedha hizo.

Vilevile, wajumbe walishauri kuwa gari la Halmashauri liendelee kufanya kazi ya uzoaji wa taka katika Mitaa, wakati mchakato wa ubinafsishaji wa chanzo cha usafi wa mazingira ukiendelea kufanyiwa kazi. Taarifa ya Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**III. Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya VVU na UKIMWI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU aliwasilisha taarifa ya utakelezaji wa shughuli za Kamati mbele ya wajumbe wa kikao, ambapo alieleza kuwa Kamati hiyo inajumuisha Divisheni mbili ambazo ni Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe na Maendeleo ya Jamii. Alieleza kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 19/01/2023 na


CamScanner

kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba – Disemba, 2022/2023.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU ilipokelewa na kuiridhiwa na wajumbe.

## IV. Kamati ya Fedha na Utawala

Kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Utawala Mhe. Diwani ambaye ni mjumbe wa Kamati aliwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya wajumbe wa kikao cha Baraza ambapo alieleza kuwa Kamati inajumuisha Divisheni na Vitengo sita ambazo ni Divisheni ya Mipango na Uratibu, Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Huduma za Sheria, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Kitengo cha Fedha na Uhasibu na Kitengo cha TEHAMA na Takwimu. Alieleza kuwa Kamati iliketi vikao vyake tarehe 29/11/2022, 29/12/2022 na 27/01/2023 kujadili na kupitisha masuala mbalimbali pamoja na taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba - Disemba, 2022. Hivyo, alichanganua taarifa ya mapato na matumizi pamoja na fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa kama ifuatavyo:-

### a) Mapato na matumizi

Ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Mji wa Kondoa imejiwekea lengo la kukusanya shilingi **19,912,978,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Halmashauri ilivuka na bakaa ya kiasi cha shilingi **785,078,798.00** na kupelekea bajeti ya utekelezaji kuwa shilingi **20,698,056,798.00**

Aidha, katika kipindi cha mwezi Disemba, 2022 Halmashauri imekusanya kiasi cha shilingi 2,285,349,433.48 na kufanya Jumla ya Makusanyo yote kuishia 31/12/2022 kuwa kiasi cha shilingi 8,557,362,349.82 sawa na asilimia 43% ya makisio ya mapato kwa mwaka 2022/2023. Mapato hayo yaliainishwa kama ifuatavyo;-

| | | |
|---|---|---|
| i. Mapato ya ndani halisi | - | 481,424,736.30 |
| ii. Mapato ya Kisekta | - | 235,237,672.63 |
| iii. Ruzuku ya Serikali Kuu (OC) | - | 716,662,408.93 |

iv. Ruzuku ya Serikali Kuu Mishahara - 5,005,795,990.00

v. Miradi ya Maendeleo - 2,548,163,898.73

Vilevile ilielezwa kuwa Halmashauri imekisia kutumia kiasi cha shilingi 19,912,978,000 kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kutoka vyanzo mbalimbali ikijumuishwa na bakaa ya mwaka 2021/2022 ya Shilingi 785,078,798.00 na kufanya jumla ya makisio ya matumizi kuwa shilingi 20,698,056,798.00. Aidha, kwa kipindi cha Mwezi Disemba, 2022 Halmashauri ya Mji Kondoa imetumia kiasi cha Shilingi 1,494,160,134.04 na kufanya Jumla ya Matumizi kuishia 31/12/2022 kuwa kiasi cha shilingi 7,091,111,404.68 ikiwa ni sawa na asilimia 36 ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Matumizi hayo yaliainishwa kama ifuatavyo;-

i. Vyanzo vya mapato ya ndani halisi - 452,342,523.52

ii. Mapato ya kisekta - 201,519,248.29

iii. Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) - 288,259,464.20

iv. Ruzuku ya Mishahara - 4,999,923,500.00

v. Miradi ya Maendeleo - 1,149,066,668.67

**b). Mapokezi ya fedha na utekelezaji wa miradi**

Ilielezwa kuwa Katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023, Halmashauri iliidhinishiwa shilingi 6,252,135,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao;-

| Na | Chanzo cha Fedha | Fedha Idhinishwa kwa mwaka 2022/23 | Fedha Pokelewa hadi Disemba, 2022 | Fedha tumika hadi Disemba, 2022 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ELIMU BILA MALIPO | 758,930,000.99 | 421,627,678.76 | 421,627,678.76 |
| 2 | EGPAF | 57,810,000.00 | | |
| 3 | GLOBAL FUND | 14,169,000.00 | 2,450,000.00 | 2,450,000.00 |
| 4 | UNICEF-POLIO | 10,000,000.00 | 11,945,250.00 | 11,945,250.00 |
| 5 | TASAF | 1,052,819,000.00 | 241,704,101.00 | 241,704,101.00 |
| 6 | CHANJO | 45,471,000.00 | | |
| 7 | HEALTH BUSKET FUND | 107,918,000.00 | | |



CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8 | EP4R | | 250,000,000.00 | 59,314,000.00 |
| 9 | SEQUIP | 573,000,000.00 | | |
| 10 | SERIKALI KUU | 1,834,250,000.00 | 1,634,250,000.00 | 27,968,200.00 |
| 11 | S/KUU (NJE BAJETI) | | 180,000,000.00 | 180,000,000.00 |
| 12 | MFUKO WA JIMBO | 50,386,000.00 | 50,386,000.00 | |
| 13 | MITIHANI | 400,816,000.00 | 247,357,000.00 | 247,357,000.00 |
| 14 | LISHE | 56,566,000.00 | | |
| 15 | BOOST | 1,290,000,000.00 | | |
| 16 | NTD | | 8,704,494.00 | 8,704,494.00 |
| | **JUMLA** | **6,252,135,000.00** | **3,048,424,523.76** | **1,201,070,723.76** |

Hadi kufikia mwezi Disemba, 2022, Halmashauri imepokea kiasi cha shilingi 3,048,424,523.76 kutoka katika vyanzo mbalimbali ambapo kiasi cha shilingi 2,533,620,678.76 ni fedha kutoka Serikali Kuu na shilingi 514,803,845.00 kutoka kwa wahisani. Aidha, kiasi cha shilingi 430,000,000.00 kimepokelewa nje ya Bajeti.

Halmashauri imekuwa ikitenga asilimia 40 ya mapato yake ya ndani (Mapato Halisi) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga jumla ya shilingi 348,920,000.00.

Aidha hadi kufikia mwezi Disemba, 2022 kiasi cha shilingi 84,145,000.00 kimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu.

**Matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo**

Hadi kufikia mwezi Disemba, 2022 Halmashauri ya Mji Kondoa imetumia kiasi cha shilingi 1,201,070,723.76 katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo (shilingi 876,952,878.76 kutoka Serikali Kuu na shilingi 324,117,845.00 kutoka kwa Wahisani.) Mchanganuo wa Matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo;-

i. Fedha za Mapato ya ndani shilingi 135,145,000.00
ii. Shillingi 22,000,000.00 zimepelekwa kwenye vikundi vya wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu
iii. Shilingi 113,145,000.00 zimetolewa kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo



CamScanner

Aidha, fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha shilingi 2,533,620,678.76 zilipokelewa na zilishapelekwa maeneo husika, pia kiasi cha shilingi 247,357,000.00 kilipokelewa kwa ajili ya shughuli za Mitihani na kiasi cha shilingi 421,627,678.76 zilipokelewa kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira ya kufundisha na kujifunzia kwa shule za Msingi na Sekondari.

Vilevile, fedha kutoka kwa wahisani kiasi cha shilingi 241,704,101.00 zimepelekwa maeneo husika kwa ajili ya kuwezesha kaya masikini.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kisha ilihojiwa kuhusu ununuzi wa eneo la ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkurugenzi kugharimu kiasi kikubwa cha fedha kwa hekari moja. Ufafanuzi ulitolewa ni mchakato wa awali na suala hilo lilirejeshwa kwenye Menejimenti kwa ajili ya kulichakata upya na tayari timu ya ufuatiliaji imeundwa kwa ajili ya kufanya mazungumzo na mwenye eneo ili bei ipungue.

Aidha, wajumbe walihoji kuhusu kutowasilishwa kwa mifuko 636 ya saruji katika kituo cha Afya Serya. Ufafanuzi ulitolewa kuwa mifuko hiyo iliwasilishwa na wahusika wa kituo cha Serya walikiri kuipokea mifuko hiyo isipokuwa utunzaji wa nyaraka haukuzingatiwa na kupekelea kupata hoja ya ukaguzi.

Pia wajumbe walihoji kuhusu Menejimenti kutotumia eneo ya wazi ili kuongeza mapato kama vile eneo la bucha ya zamani liliopo Mtaa wa Ubembeni katika Kata ya Chemchem. Ufafanuzi ulitolewa kuwa maombi yaliyowasilishwa Halmashauri ni ya wananchi wawili ambao waliomba eneo hilo kwa ajili ya kufanya biashara. Mwananchi aliyeomba kwa ajili ya kuendesha shughuli ya uchomeleaji ambaye wajumbe waliridhia kupewa eneo hilo hadi sasa hakujitokeza kwa ajili ya kujaza mkataba. Hivyo ilishauriwa kuendelea kutangaza eneo hilo kwa wananchi wenye uhitaji wa kuwekeza.

Aidha, ilihojiwa kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa eneo la ujenzi wa vibanda kwa wananchi ambao wameomba na wamekosa. Ufafanuzi ulitolewa kuwa hakuna mwombaji aliyekosa eneo la ujenzi wa kibanda kwani maombi yote yalipokelewa na kupitishwa hivyo,watatakiwa kufika kwa Afisa sheria wa Halmashauri ili kupatiwa mikataba.

Aidha, ilihojiwa ni lini Halmashauri ya Mji itakabidhi wananchi eneo la Soko lililopo Kata ya Kilimani ili kuanza ujenzi wa soko hilo na wananchi wapate huduma ili kupunguza usumbufu kwa wananchi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala hilo limepokelewa na Menejimenti kwa ajili ya kulifanyia kazi.



CamScanner

Wajumbe walihoji kuhusu sababu inayopelekea kushuka kwa makusanyo ya mapato yatokanayo na vibali vya ujenzi . Ufafanuzi ulitolewa kumekuwa na changamoto ya ukusanyaji wa vibali vya ujenzi, hivyo kuanzia sasa vibali vyote vya ujenzi vitaingizwa kwenye Mashine za kukusanyia mapato (POS) ili iwe rahisi kwa watendaji kukusanya pia kupunguza usumbufu kwa wananchi.

Wajumbe walishauri Menejimenti kuimarisha vyanzo vya mapato ili kuongeza mapato ya Halmashauri kwa kuongeza ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato (POS) pamoja na kufungua stendi kuu ya mabasi Bicha. Ilifafanuliwa kuwa Halmashauri imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa stendi inakamilika na kufunguliwa pia mashine za kukusanyia mapato (POS) zilizopo zinatosheleza na mbovu zipo kwenye utaratibu wa kuziondoa kwenye mfumo. Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**MUHT NA 20/2022/2023 TAARIFA MBALIMBALI KUTOKA KWA MKURUGENZI NA MHE. MWENYEKITI.**

Mwenyekiti alisisitiza yafuatayo kufanyiwa kazi;-

i. Waheshimiwa Madiwani kuwa karibu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.
ii. Kamati za ujenzi wa miradi kuwa na taarifa zote zinazohusu mradi husika.
iii. Waheshimiwa Madiwani wasisite kutoa taarifa juu ya ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi. Pia kusimamia matumizi sahihi ya fedha pamoja na utunzaji mzuri wa nyaraka.
iv. Alisisitiza kuongeza nguvu katika suala la elimu na kuhakikisha madawati yanapatikana ya kutosha katika kila Shule ambazo zina upungufu wa madawati ili kuepuka wanafunzi kukaa chini. Pia kuona namna ya kuongeza Shule nyingine ya Msingi katika maeneo ya mjini ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi kwenye shule.
v. Kufanyika msawazo wa walimu kulingana na upungufu uliopo katika shule kulingana na idadi ya wanafunzi.

**MUHT NA 19/2022/2023 MASUALA YA KIUTUMISHI**

Baraza lilijigeuza kamati na kupitisha taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya watumishi na mrejesho wa masuala yaliyopitishwa ulitolewa kwenye kikao cha Baraza. Ambapo ilielezwa kuwa kamati iliridhia na kumthibitisha kazini Ndg. Jeremiah Longido pamoja na kuridhia

kuajiriwa kwa watumishi wa mkataba wawili ambao ni Ndg. Stanley D. Robert na Ndg. Khalifa Lubuva. Taarifa hiyo ilipokelewa na kuridhiwa kupitishwa na Baraza kwa hatua za kiutekelezaji.

**TAARIFA KUTOKA TAKUKURU**

Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Kondoa alitambulisha mradi mpya unaojulikana kama TAKUKURU rafiki ambao unalenga kuimarisha masuala ya utawala bora. Pia ilielezwa kuwa kero zote za wananchi zitatatuliwa katika ngazi za kata na mchakato mzima wa utatuzi utafuatiliwa na ngazi ya TAKUKURU Wilaya ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi.

**NASAHA KUTOKA KWA MWENYEKITI WA CHAMA CHA MAPINDUZI**

Alitoa pongezi kwa Waheshimiwa Madiwani kwa kujadili vizuri agenda zilizowasilishwa hasa katika suala la kusimamia ukusanyaji na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato. Pia alisisitiza Waheshimiwa Madiwani kutembelea shule zilizopo katika maeneo yao kubaini changamoto zinazowakabili walimu ili kushirikiana kwa pamoja na kuzitafutia ufumbuzi na kuongeza ufaulu.

Aidha, alisisitiza kuwa fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zitumike kwa wakati. Pia ilishauriwa Wakuu wa Divisheni na Vitengo kuwashirikisha viongozi waliopo katika kamati za miradi pamoja na kuwajengea uelewa wa kutosha katika usimamizi wa miradi hiyo na kupewa nafasi katika miradi wanayosimamia.

Waheshimiwa Madiwani walisisitizwa kuwaeleza wananchi mafanikio yote yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya sita ili kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu juhudi na kazi zinazofanywa na Serikali yao.

**MUHT NA 21/2022/2023KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti kabla ya kufunga aliwashukuru wajumbe wote kwa mawazo yenye tija na aliagiza Menejimenti kufanya utafiti ili kubainisha sababu zilizopelekea kushuka kwa ufaulu katika matokeo ya mitihani ya Kitaifa iliyofanyika mwaka 2022 kwa baadhi ya Shule za Sekondari na kupendekeza nini kifanyike ili kuinua ufaulu katika Shule hizo. Pia alisisitiza Kamati za mazingira kusimamia usafi wa mazingira pamoja na watumishi wa afya kuwa karibu na wananchi ili kushughulikia kero za wananchi. Aidha, alishukuru vyombo vya ulinzi na usalama



CamScanner

kwa kuimarisha suala zima la ulinzi na usalama. Aliwatakia safari njema warejeapo majumbani mwao alifunga kikao saa 08 : 25 mchana.

**Umet hibitishwa**

............................ ............................

Jina...Desgnatus IRW... Jina...MOHAMED KIBERENGE...

**Katibu** **Mwenyekiti**

28.04.2023
..........................

**Tarehe.**



CamScanner